

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.LDC/L.10/13 VOL.V/04**

**Tarehe. 25/05/2022**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA  
ANATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:-**

**KATIBU MAHSUSI (PERSONAL SECRETARY) III – NGAZI YA MSHAHARA  
TGS B (NAFASI 4)**

**1. SIFA ZA KUAJIRIWA**

- i) Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV au VI
- ii) Wawe wamehudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu.
- iii) Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na
- iv) Wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na serikali na kupata cheti katika program za Wondows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

**2. KAZI NA MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI (PERSONAL SECRETARY) III**

- i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- ii) Kusaidiakupokea wageni na kuwasailishida zaona kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii) Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za kikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- iv) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, Nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini
- v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa Wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na Wasaidizi hao
- vi) Kusaidia kupokea Majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
- vii) Kufanya kazi nyingine zozote atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi



## DEREVA II – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 4)

### 1. SIFA ZA KUAJIRIWA

- i) Kuajiriwa wahitimu wenye cheti cha Mtihani wa Kidato cha IV au VI,
- ii) Wawe mwenye Leseni daraja "C" au "E" ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali,
- iii) Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- iv) Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

### 2. KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA II

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii) Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika
- iv) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- v) Kujaza na kutunza taarifa zote za safari katika daftari la safari "Log-book"
- vi) Kufanya usafi wa gari
- vii) Kufanya kazi nyingine zozote atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi


## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

- i) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 hadi 45.
- ii) Waombaji wote wanatakiwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- iii) **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- iv) Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- v) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- vi) Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.
- vii) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa ya kazi husika na picha mbili "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma. Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
- viii) **"Transcripts", "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV and FORM VI results slips) Havitakubaliwa.**

- ix) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- x) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 08/06/2022 saa 09:30 Alasiri.
- xi) Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yatumwe Posta yakiwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA,  
S.L.P 19,  
LUDEWA.**

Tangazo hili limetolewa na:-

  
Sunday N. Deogratius  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
**LUDEWA.**

**Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
Ludewa**

Nakala: Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P 2320,  
**DODOMA.**